**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Shule ya sekondari Zunzuli**
**S . L . P 16, Shinyanga**
**TAREHE……………**

Namba za walimu
Mkuu wa shule: 0621 226577
Makamu mkuu wa shule: 0628 391 670
Mwalimu wa malezi:0628 381 090
Kumb Na……………………………

**Jina La Mwanafunzi………………………………………………………………..**
**S. L .P ………………………..**
**……………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZUNZULI WILAYA YA SHINYANGA MKOA WA SHINYANGA MWAKA……………..**

- **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2026.Shule ya sekondari Zunzuli ipo umbali wa km 94 Kaskazinini/Mashariki/Magharibi/Kusini mwa makao makuu ya mkoa/halmashauri ya wilaya ya Shinyanga.Usafiri wa basi kutoka mjini Shinyanga unapatikana katika kituo cha mabasi cha stendi ya zamani .Nauli ni Tsh 7,000/= Panda mabasi ya Salawe shuka kituo cha Ikonongo baada ya kushuka chukua bodaboda itakayokuleta mpaka shuleni Zunzuli sekondari nauli ni Tsh. 2,000/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe ………………. na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………………..

## 2.0 MASOMO YAFUNDISHWAYO

- **KISWAHILI**
- **GEOGRAPHY**
- **HISTORY**
- **ENGLISH LANGUEGE**
- **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**
- **ACADEMIC COMMUNICATION**

## 2.1 SARE ZA SHULE

### A.WAVULANA

i. Suruali (2) rangi ya dark blue ,ushonaji mfuko mmoja wa nyuma usibandikwe,suruali isiwe fupi isiyobana na iwe na turn up pamoja na marinda

ii. Shati mbili(2) nyeupe mikono mirefu ziwe na mfuko mmoja.

iii. Tai rangi ya dark blue iwe ndefu

iv. Viatu vyeusi vya kamba visiwe na visigino virefu wala buti

v. Soksi nyeusi jozi mbili

vi. Mkanda wa suruali mweusi usiwe na pini kubwa wala mpana sana usizidi sm 5

vii. T-shirt dark blue (inapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=)

### B.WASICHANA

i. Sketi 2 rangi ya dark blue iwe na marinda madogo na mikanda miwili na iwe ndefu ifike kwenye kifundo cha mguu (pia zina patikana mazingira ya shule kwa Tsh. 40,000/=) kwa atakayehitaji

ii. Shati mbili (2) nyeupe mikono mirefu kila shati liwe mfuko mmoja kifuani mkono wa kushoto, kwa waislamu aje nusu kanzu mbili .

iii. Tai rangi ya dark blue iwe ndefu (rangi ya sketi)

iv. Soksi nyeupe jozi 2 ziwe ndefu

v. Viatu jozi 2 vya ngozi rangi nyeusi vyenye visigino vifupi kufunika miguu na viwe na kamba

vi. Hijabu mbili nyeupe , mbili dark blue na nyekundu moja .

vii. T-shirt dark blue (inapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=) kwa atakayehitaji

- **SARE ZA MICHEZO**

i. Traki suti rangi nyekundu yenye ufito mweupe kwa wote(pia zina patikana mazingira ya shule kwa Tsh. 30,000/= kwa atakayehitaji)

ii. Bukta na T-shirt rangi ya bluu yenye ufito mweupe kwa wote

iii. Viatu vya raba rangi yoyote kwa wote

**Zingatio**: kwa mwanafunzi aliyekuwa mwanachama wa skauti na anapenda kuendelea aje na sare za skauti

2.2 **Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na, 307011000374 , yenye jina la Zunzuli Sekondari , katika Benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

**Zingatia:** Kila mzazi/mlezi amkatie mwanae bima ya afya ya NHIF ya Tsh. 50,400/= kwa mwaka au alipe shuleni kiasi cha Tsh. 50,400/= taslimu na mwanafunzi mwenye umri wa miaka 18+ awe na namba ya utambulisho wa taifa (NIDA) kwa ajili ya bima hiyo na kama hana namba ya NIDA fedha haitopokelewa. Kwa mwanafunzi ambaye tayari ana bima ya NHIF aje na kadi na mchango wa Tsh. 50,400/= hautamhusu.

**2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni kama ifuatavyo:**

i) Ream ya karatasi 2 (kwa mwaka). Ziwe za A4 (Double A)

ii) Vitabu vya masomo ya taasusi husika (angalia orodha ya vitabu iliyoambatanishwa).

iv) Scientific calculator kwa masomo ya sayansi, Geography na hesabu

v) Godoro futi 3 , linapatikana shuleni kwa Tsh . 95,000/=(elfu tisini na tano tu kwa atakayehitaji).

vi) Mashuka manne (4); 2 Bluu na 2 Pinki tu bila maua , mto 1 (mto sio lazima), chandarua 1 pembe nne rangi yoyote.

vii) Vyombo vya chakula sahani 1 ; bakuli 1; kijiko 1 na kikombe1.

viii) Ndoo mbili, kubwa moja ndogo moja zenye mifuniko.

ix) Kwanja ,jembe na mpini wake kwa tahasusi ya HKL

(x) Reki 1, Panga 1,Mkasi wa mauwa 1 kwa tahasusi ya HGK

(xi) SQUIZER 1, Sostbroom, Hardbroom 1, ufagio mrefu wa Chelewa kwa wote

(xii) sabuni ya maji lita 2 na brush kwa ajili ya usafi wa choo

xiii) Spring file 1

XIV) Gauni la kushindia, linaptikana shuleni kwa Tsh . 24,000/= kwa atakayehitaji

NB , Pia vifaa hivi vinapatikana mazingira ya Shule kwa bei ya kawaida.

- **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu,sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Rais **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:-

(a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunziwengine na jamii kwa ujmla ni jambo la lazima

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(morning and evening preparation)

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako

(f) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h) Kuzingatia ratiba ya shule  wakati wote

(i) Kutunza mali za umma

(j) Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki vifaa vya ncha kali na dawa bila idhini ya daktari au Muuguzi wa shule

(k) Ni marufuku kwa mwanafunzi kufika kwenye nyumba za walimu bila ruhusa ya mkuu wa shule au mlezi

**3. MAKOSA YAFUATAYO YAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

(a) Wizi

(b) Uasherati,Kuoa au kuolewa na mahusiano ya jinsia moja

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika

(e) Kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kudharau wimbo na bendera ya taifa

(h) Kuwa mjazito/kupata mimba

(i) Kutoa mimba

(j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

(k) Kukataa adhabu kwa makusudi

(l) Kuwa na simu ya mkononi

(m) Utoro

(n) kufuga ndevu

(o) kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu

(p) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wagen

**MUHIMU**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayerusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kweni Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)

**3.1 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

(a) Medical Examination Form,ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.Fomu hii itakabdhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d)Wakati wa kuripoti mwanafunzi awasilishe nakala(photocopies) za matokeo ya kidato cha nne(result slip) na cheti cha kuzaliwa(birth certificate) Bandika picha za wazazi/walezi kama inavyoelekezwa kwenye KIAMBATISHO B ukurasa wa 8, Aidha picha(passport size) ya mwanafunzi ibandikwe upande wa juu kulia kwenye fomu hiyo(KIAMBATISHO B) ukurasa wa 8.

NB: Hakikisha viambatanisho vyote vinavyotakiwa kujazwa vimejazwa kwa usahihi na kukabidhiwa shuleni wakati wa kuripoti.

**5.1** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU***

***………………………………………………….***

***GEORGE E. ULOMI***

***MKUU WA SHULE***

**0621226577 au 0764896577**

**ANGALIZO**: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa .

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: 0621 226577
- Makamu mkuu wa shule: 0628 391 670

- Mwalimu wa malezi:0628 381 090
- Mwandamizi Taaluma: 0756442366

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi …………………………………..mzazi/mlezi wa …………………………..nimezisoma sheria za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na amezielewa. Ninakubaliana kushirikiana na uongozi wa Shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya mzazi/mlezi………………………………tarehe………………………………

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………..wa kidato cha ……….. nimesoma kwa makini sheria na taratibu za Shule nikiwa na mzazi/mlezi wangu. Nimejadiliana naye na nimeelezwa vizuri kabisa. Ninaahidi kuwa nitazifuata na endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na taratibu hizi hatua zichukuliwe dhidi yangu. Ewe mwenyezi Mungu nisaidie.

Saini ya mwanafunzi…………………………….Tarehe ……………………………

Ni imani yangu kuwa utafuata hizi sheria ili uweze kujifunza kwa bidii na kwa mafanikio yaliyo bora.

Nakutakia kila la heri na karibu sana Zunzuli Sekondari.

………………………………………………………

**GEORGE E. ULOMI**

**MKUU WA SHULE**

**0621226577 au 0764896577**

KIAMBATISHO B

Shule ya Sekondari Zunzuli S. L. P 16,Shinyanga. Simu: 0621226577/0764896577

Barua pepe: zunzulisec@gmail.com

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi…………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………

3. Mahali alipozaliwa:

Mkoa………………………Wilaya……………………………….Tarafa……………………………Kata………… ………Kijiji/Mtaa………..................

4. Dini………………………………… Dhehebu…………………………………………

5. Jina la baba mzazi/mlezi……………………………………………… Anuani……………………….. Namba ya

simu……………………….. Kazi ya baba mzazi/mlezi…………………………………………… Yuko hai? Ndiyo/ Hapana (kata isiyohusika)

6. Jina la mama mzazi/mlezi……………………………………………….Anuani ……………………

Namba ya simu……………………………………kazi ya mama mzazi/mlezi……………………………… Yuko hai? Ndiyo/Hapana (kata isiyohusika)

Bandika picha ya baba/mlezi

Bandika picha ya mama/mlenzi

7. Ndugu wa karibu aliyeridhiwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa/matatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.

Jina kamili…………………………………………Anuani……………………….. Namba ya simu…………………………………… Kazi yake ………………………uhusiano na mwanafunzi…………………………..

Bandika picha ya ndugu wa karibu

KIAMBATISHO C

MEDICAL EXAMINATION FORM

NAMEO F STUDENT…………………………………………………………………….

To medical officer I/C of

………………………………………..District/ Regional/Referral/Designated Hospital,

P.O BOX…………………………..

Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for being able to pursue two years of Secondary School Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-

i. Blood pressure………………………………………………………………

ii. Sickle cell test…………………………………………………………………..

iii. (a) Eyesight…………………………………………………………………..

(b) Spleen……………………………………………………………………………...

(c) Hearing…………………………………………………………………………..

(d) Veneral diseases………………………………………………………………..

(e) Lepsory…………………………………………………………………………..

(f) Typhoid…………………………………………………………………………

iv. Neuroses…………………………………………………………………………….

v. Other serious disease……………………………………………………………

General comment(s)…………………………………………………………………..

Name……………………………………………………………………………….

Designation…………………………………………………………………………

Official stamp…………………………… Date……………………………………

ANGALIZO: mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na saini ya Mganga.

Atakayegundulika kuwa hakuchukua vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.

KIAMBATISHO D

Shule ya Sekondari Zunzuli

S. L. P 16,Shinyanga.

Simu: 0621226577/0764896577

Barua pepe: zunzulisec@gmail.com

FOMU YA KUKUBALI NAFASI

Mimi……………………………………………nakubali nafasi ya kidato cha tano niliyopewa na Shule ya Sekondari Zunzuli. Ninaahidi kutii na kufuata kwa uaminifu sharia, kanuni na taratibu zote za shule, kujifunza kwa bidii, juhudi na maarifa kwa uwezo wangu wote ili kutimiza lengo la kufaulu kwa kiwango cha juu kwa faida yangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla. Ninaahidi kuripoti shuleni nikiwa nimevaa yunifomu kamili kama ilivyoelekezwa na kwa siku iliyopangwa bila kuchelewa.

Saini ya mwanafunzi……………………

Tarehe …………………………………

ORODHA YA VITABU VYA KIADA VINAVYOPENDEKEZWA

Ili mwanafunzi aweze kupata elimu bora na yenye kumwezesha kukabiliana na mazingira halisi ya maisha anapaswa kuwa na vitabu. Ifuatayo ni orodha pendekezwa.

1. KISWAHILI

- Dunia Uwanja Fujo – Euphrase Kezilahabi
- Ua la Faraja – w . E . Mkufya
- Mirathi ya Hatari – C.G. Mung'ong'o
- Wasifu wa Siti Binti Saad – Shaaban Robert
- Mukwava wa Uhehe - M.M , Mulokozi
- Shujaa Mirambo – Emmanuel Mbogo
- Usaliti Mjini – Francis Ibuga
- Fumbo linaloelea – Nyambari Nyagwine
- Malega wa Ziwa kuu – Wallah Bin Wallah
- Andamo , Msafiri Safarini

- Wosia wa Baba

2. HISTORY

- History form five ( Tanzania Institute of Education)
- Shibitali

3. ENGLISH LANGUAGE

- Oxford Advanced Learner's Dictationary (12th edition)
- Animal Farm – George Orwell
- Chasing the Leopard ,Findig the Lion – Julie Wakemanlinn
- The Opportunist Elite – Nyambari C. Nyangwine
- The Horizon Unveiled – Fellowes Mwaisela
- The Govermment Inspector – Nikolai V . Gogol
- An Enemy of the people – Henrik Ibsen
- A Taste of Heaven – Farouk Topan
- Summons ; Poem From Tanzania - Richard S. Mabala
- Poets of Africa ; Lament of the Silent $ Other poem – Jared Angira

4. GEOGRAPHY

- General geography in diagrams – R.E Bunnet
- Practical geography for Africa – John M.Pritchard
- Practical Geography for Advanced level (Tanzania Instute of Education )
- Physical Geography for Advanced level ( Tanzania Institute of Education)

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISRATION&LOCAL GOVERNMENT**
**ZUNZULI SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION**

1. STUDENT NAME…………………………………………………………………..
2. AGE…………………..HEIGHT (CM)……………...WEIGHT (KG)……………..
3. BLOOD EXAMINATION: HEMOGLOBIN…………..BLOOD GROUP………..
4. ANY ABNORMALITIES NOTED ………………………………………………
5. STOOL EXAMINATION………………………………………………………..
6. URINALYSIS…………………………………………………………………….
7. T.B TEST (IF NEGATIVE, WAS IMMUNIZATION GIVEN)……………………
8. EYES ……………………………………………………………………………..
9. CHEST……………………………………………………………………………
10. ANY CHRONIC COMPLAINTS NOT NOTED ABOVE EG

    a) ASTHMA……………………………………………………..
    b) HEADACHE…………………………………………………….
    c) INABILITY TO EAT CERTAIN FOOD…………………………
    d) SKIN DISEASE E.T.C……………………………………………..
    ………………………………………………………………………...

11. Also anything that the school health staff should know about
    ----------------------------------------------------------------------------------------------------
    ----------------------------------------------------------------------------------------------------
12. Any treatment given or recommended__________________________________________
    ____________________________________________________________________
    ____________________________________________________________________
    ____________________________________________________________________

**NOTE**: If any examinations requested above cannot be carried out, it is useful if it is noted that they have not been done rather than wring NAD down

In case of Bilharzia it is recommended that students attend the Bilharzias as clinic before they come to school,

**SIGNATURE OF EXAMINER………………………………**

**DESIGNATION………………………………………………**

**DATE……………………… STATION………………….**